

JINA \_\_\_\_\_ DARASA \_\_\_\_\_

SAHIHI \_\_\_\_\_ TAREHE \_\_\_\_\_

102

KISWAHILI

KIDATO CHA KWANZA

MUDA:  $2\frac{1}{2}$

## **MAAGIZO**

Karatasi hii ina sehemu tano **A, B, C, D** na **E**. Hakikisha umejibu maswali yote katika kila sehemu.

<b>SEHEMU</b>		<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
A	UFAHAMU	20	
B	MATUMIZI YA LUGHA	30	
C	ISIMU-JAMII	10	
D	FASIHI SIMULIZI	20	
E	USHAIRI	20	
	<b>JUMLA</b>	<b>100</b>	

Karatasi hii ina kurasa 7 zilizopigwa chapa.

## SEHEMU YA A: UFAHAMU

### Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali

Ualimu ni kazi inayopendwa na wengi ingawa huwa na changamoto nyingi. Mimi nilipohitimu kuwa mwalimu wa shule ya chekechea, nilifurahi hadi gego la mwisho likaonekana. Nilidhani ndoto yangu ya miaka ilikuwa imetimia. Niliona ningeweza kufanya mambo mengi ambayo walimu watangulizi wangu walikuwa wakiyafanya.

Nilipata nyota ya jaha kwa kupata kazi jijini katika shule ya chekechea ya Sadikika. Nilikuwa nimeyasikia mengi kuhusu watoto wa jijini; wengi wao hufikiriwa kuwa watovu wa nidhamu. Hivyo basi, nilianza kutayarisha kijiboko change cha kuwanyamazishia wanafunzi wangu darasani. Nilijaribu kujitandika kwa kijiboko hicho nikiona kinafaa; hakingempa mwanafunzi wa shule ya chekechea maumivu mengi.

Shuleni Sadikika nilikaribishwa vizuri na walimu wenzangu. Sikuwa nimekibeba kile kijiboko kwani nilitaka kuchunguza mambo yalivyoendeshwa huko. Nilishangaa kuona kuwa hakukuwa na mwalimu yeyote aliyekuwa na kijiboko. Hata hivyo, sikutaka kujitilia kitumbua mchanga kwa kuhojihoji mambo. Walimu wenzangu, mkuu wa idara na mwalimu mkuu walinipa mawaidha kuhusu shule na kazi. Hawakunitaja lolote kuhusu nidhamu.

Siku ya pili nilikiweka kijiboko change mkobani. Niliingia katika dara niliotengewa na kuvipata vitoto vya umri wa miaka mitano hivi. Vitoto vyenyewe vilikuwa vichakaramu ajabu! Baadhi yao walinishikashika na kuniambia sikuwa nimevaa vizuri kama mwalimu wao za zamani. Nikapandwa na mori. Nikavifokea na kuviambia virudi madawatini mwao vinisikilize nikifunza. Nikaviambia “Nimekuja kufundia. Nyamazeni niwafundishe!”

Watoto wote walishangaa na kutulia kama maji ya mtungi. Hapo nikaona nimegonga ndipo. Nikazungumza kidogo kasha nikaanza kuandika mambo mengi ubaoni. Nikawaambia wanakili mambo yote vitabuni. Hee! nikaona wote wananikodolea macho na kuonyesha kupigwa na bumbuazi. Mmoja aliyelitwa Mwendapole akakivunja kimya hiki. “Mwalimu tumechola! Sisi bado tu watoto.” Wenzake wakafurahi, Wakasimama na kutaka kutoka nje wakacheze.

Hapo, nikaona wakati wa kijiboko change kufanya kazi ulikuwa umefika; nikakitoa mkobani. Mara tu watoto walipoona hivyo, wakaanza kupiga kelele na wengine kulia. Nikachapachapa wachache. Wote wakakimbia, nikabaki peke yangu darasani. Nikawangoja warudi darasani; hwawakurudi.

Mkuu wa shule akanifuata na kuniuliza maswali. Hakunielewa kabisa na akaniambia angezungumza na watoto ili warudi darasani, ingawa ilibidi nibadilike na kuwa rafiki yao. Niliporudi nyumbani ilinibidi nichome hicho kijiboko change na kuapa kuwa kamwe singerudia tabia hiyo tena.

Siku iliyofuata wazazi kadhaa walifika shuleni. ‘Wambeya’ walikuwa wameshafikisha maneno nyumbani. Si msomo huo nilioupata. Nikajinyamazia kijinga. Kimoyomoyo

nilijisemea “Wazazi hawa ni wadekezaji sana, chuma chao ki motoni. Mchelea mwana kulia hulia yeye.”

Baada ya juma, hali ilikuwa shwari. Wanafunzi walianza kunikubali japo Mwendapole hakuwa mchangamfu. Kumbe alikuwa amejikojolea. Wenzake wakaanza kumcheka name nikashindwa kujizuia. Kwa pamoja, tukaanza wimbo wa ‘kikojozi’.

Mwalimu mkuu alipoyasikia hayo, alionya tena, nikabdilika na kuwa chanda na pete na wanafunzi wangu. Mui akawa mwema.

### **Maswali**

(a) Ipe taarifa uliyosoma anwani mwafaka (alama 1)

---

---

(b) Kwa nini msimulizi alitafuta kijiboko kabla ya kufika shuleni sadikika? (alama 2)

---

---

(c) Kulingana na kifungu hiki, eleza matarjio ya msimulizi (alama 3)

---

---

---

(d) (i) Msimulizi alikuwa na maana gani aliposema kuwa hakutaka ‘kujitilia kitumbua mchanga’? (alama 2)

---

---

---

(ii) Nikapandwa na mori. (alama 2)

---

---

(e) Kulingana na watoto, mwalimu alikuwa na upungufu gani? (alama 3)

---

---

---

(f) Kwa nini wazazi walifika shuleni? Toa sababu mbili. (alama 2)

---

---

(g) Kwa nini mwalimu aliamua kukichoma kijiboko chake? (alama 2)

---

---

---

(h) Kwa mujibu wa kifungu, ni nini maana ya methali 'mchelea mwana kulia hulia yeye?' (alama 2)

---

---

---

(i) Andika maana ya kifungu kifuatacho kama kilivyotumika katika taarifa. Nimegonga ndipo (alama 1)

---

---

---

(j) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama uvlivyotumika katika kifungu (alama 2)  
(i) Changamoto

---

---

---

(ii) Vichakaramu

---

---

---

**SEHEMU YA B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Huku ukitoa mfano eleza tofauti kati ya sauti hafifu. (alama 2)

---

---

---

(ii) Sauti ghuna

(b) Taja sifa bainifu za sauti zifuatazo (alama 2)

(i) /e/

(ii) /ngʔ/

(c) (i) Kiimbo ni nini? (alama 1)

---

---

---

(ii) Kwa kuzingatia kiimbo toa mifano miwili ya sentensi zitokanazo na kiimbo (alama 2)

---

---

(d) **Kanusha:** (alama 2)

(i) Msomi alituzwa siku hiyo

---

(ii) Ukisoma kwa bidii utafaulu

---

(e) Maneno haya yako katika ngeli gani? (alama 2)

(i) **chumvi** \_\_\_\_\_

(ii) **Mahaba** \_\_\_\_\_

(f) **Sahihisha sentensi,ifuatayo:** (alama 2)

Manywele ya msichana huu yamechanwa mzuri

---

(g) Andika kinyume cha: nuka (alama 1)

---

(h) Tambua aina za maneno yaliyopigwa mstari. (alama 2)

**Yeye** ni mwanafunzi hodari **sana**.

(i) Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya maneno yafuatayo: (alama 2)

(i) **Tega** \_\_\_\_\_

(ii) **Teka** \_\_\_\_\_

(j) Huku ukitoa mfano,taja matumizi mawili ya alama ya hisi (!) (alama 2)

---

---

(k) Eleza maana **mbili** za sentensi hii: (alama 2)

Bi Asha alimpigia Ali simu.

---

---

(l) Kibogoyo ni kwa meno \_\_\_\_\_ ni kwa mgongo.(alama 1)

(m) Andika sentensi ifuatayo bila kutumia '**amba**'. (alama 2)

Mti ambao unapendeza ni ule wenye matunda ambayo ni makubwa.

- (n) **Andika katika wingi.** (alama 2)  
Uta huu ni mfupi na mzito kuliko ule

- (o) **Akifisha:** (alama 2)  
Alisafiri siku ya jumapili tarehe ishiri mwezi wa Januari mwaka wa elfu mbili kumi na saba.

- (p) Kwa kutolea mfano eleza muundo mmoja wa silabi. (alama 1)

**SEHEMU YA C: ISIMU –JAMII (ALAMA 10)**

- (a) Eleza maana ya Isimu Jamii. (alama 2)

- (b) Taja sifa **tano** bainifu ya 'sajili' ya magazeti. (alama 5)

- (c) Eleza jinsi kaida zifuatazo hutawala mazungumzo katika jamii (alama 3)

(i) Uhusiano \_\_\_\_\_

(ii) Umri \_\_\_\_\_

(iii) Cheo \_\_\_\_\_

**SEHEMU YA D: FASISHI SIMULIZI**

- (a) Eleza maana ya Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi. (alama 2)

---

---

(b) Eleza majukumu matano ya **Fasihi simulizi**. (alama 5)

---

---

---

---

(c) (i) Semi ni nini? (alama 1)

---

(ii) Taja vipera vya semi. (alama 4)

---

---

---

---

(d) (i) ngano ni nini? (alama 1)

---

(ii) Fafanua sifa zozote **nne** za ngano. (alama 4)

---

---

---

---

(e) Taja tofauti tatu kati ya **fasihi simulizi** na **fasihi andishi** (alama 3)

---

---

---

---

fro free pastpapers visit: [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)